
# Mpangilio Takatifu wa Maisha

Adrian Ebens



# Mpangilio Takatifu wa Maisha

*Huleta mafanikio katika maisha yako, mawazo na mahusiano*

Adrian Ebens

Kimechapishwa na

MARANATHA MEDIA

maranathamedia-kenya.com
Fatheroflove.info
adrian@life-matters.org

# Yaliyomo


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Jitihada | 4 |
| 2. | Tufaha Iliyoanguka | 6 |
| 3. | Akisimama Juu ya Mwezi Akivikwa Jua | 9 |
| 4. | Ramani na Dira ya KIroho | 13 |
| 5. | Mpangilio Takatifu | 18 |
| 6. | Kijito Cha Uzima | 25 |
| 7. | "Mungu wa Ulimwengu huu" na Kuzaliwa kwa Nguvu Pinzani | 29 |
| 8. | Sabato kwa Nafsi: Kupata Pumziko la Ndani | 34 |
| 9. | Njia Nyembamba ya Kwenda kwa Mpangilio Takatifu | 38 |
| 10. | Hatua Ifuatayo | 43 |



## 1. Jitihada

Mwishoni mwa karne ya kumi na saba Isaac Newton alikuwa akiwaza kuhusu hali ya ufundi wa mbingu. Kulikuwa na uhusiano upi kati ya maumbile ya mbinguni jinsi yalivyozunguka mbingu? Kunaweza kuwa na sheria rahisi ya jumla ambayo ilielezea na kutawala mahusiano haya? Au ulikuwa mfumo mgumu wa ajabu zaidi ya uwezo wetu kufahamu? Ni nini kilisababisha jitihada hii katika moyo wa Newton? Je, alikuwa kwa kweli amegongwa kichwani kwa tufaha na kumsababisha kufikiria kuhusu mvutano? Ugunduzi wa hivi karibuni unaopatikana katika “London’s Royal Society” ulidhihirisha kwamba majibu katika muswada ambao ungekuwa wasifu wa maisha ya Bwana Isaac Newton.

> Baada ya chajio, hali ya hewa ikiwa joto, tulienda katika bustani na tukanywa chai, chini ya kivuli cha baadhi ya miti ya tufaha...aliniambia, alikuwa katika hali sawia, kama vile mbeleni, dhana ya mvuto (gravitation) ikamjia mawazoni. Ilifululizwa na anguko la tufaha, alipokuwa amekaa katika hali ya kuwaza. Mbona kila wakati tufaha ishuke wima kuelekea ardhini, alijiwazia yeye mwenyewe...[1]

Mtagusano huu na tufaha iliyoanguka kuliweka azimio la mfululizo wa matukio ambayo yalipelekea kuzalishwa kwa kanuni (*Principia)* ambayo

---

[1] http://www.newscientist.com/blogs/culturelab/2010/01/newtons-apple-the-real-story.html

kwayo Newton anaweka msingi wa ufundi wa jadi na sheria tatu za jumla za mwendo. Sheria hizi zinaelezea uhusiano kati ya kitu chochote, nguvu ikitenda juu yacho, na mwendo utokeao. Newton alitumia neno la Kilatini *gravitas* (uzito) kwa athari ambayo ilikuja kujulikana kama mvuto (gravity) na akaelezea sheria ya jumla ya mvuto (the law of universal gravitation).[2]

Kanuni (*Principia)* ya Newton inaweza tawala mtazamo wa kisayansi wa ulimwengu halisi kwa miaka 300 ijayo. Aliweza kutumia kanuni hizi kuelezea njia ya mwendo wa vimondo, mwendo wa mawimbi na maandamano ya jua (equinoxes) ambayo iliondoa alama yote ya mwisho kuwa dunia ilikuwa kati ya mfumo wote wa jua (solar system).[3] Utafiti wa uhusiano kati ya vitu halisi vya mbinguni ulielezea upya ufahamu wetu wa ulimwengu na kupanua uwezo wa mwanadamu kutenda kazi ndani yake, na kuunganisha nishati, ulimwengu wetu kulingana na sheria ya mvuto (laws of gravity).

Jitihada ya Newton katika vitu vya mbinguni ilichochewa na tukio lililokuwa likitendeka kati ya vitu vya duniani. Kutazama tufaha ikianguka kutoka kwenye mti kulizua swali kuhusu uhusiano uliopo kati ya tufaha na ardhi na ni nini kilizivuta pamoja.

Nikisimama katika mwisho wa karne ya 21 mawazo yangu yamegeuzwa kwa jitihada mpya – kanuni ya msingi wa vitu vya kiroho (spiritual bodies). Kama ufahamu sahihi wa vitu halisi unaweza zalisha maendeleo ya ajabu kama hayo katika jitihada za mwanadamu za kisayansi, ni athari gani inaweza kuwepo kwa ufahamu sahihi wa uhusiano baina ya vitu vya mbinguni na vitu vya kiroho vya duniani? Kwa vitu vya kiroho vya duniani narejelea uhusiano baina ya mawazo ya wanaume, wanawake, na watoto, uhusiano kati ya mwanadamu na ulimwengu takatifu na hata uhusiano katika ulimwengu takatifu. Tunaweza taja hapa kuwa jitihada za Newton zilisababishwa ndani ya nyanja ya duniani, lakini ikapata majibu yake katika nyanja ya mbinguni.

Wacha tuanze jitihada yetu ya sheria ya jumla inayotawala vitu vya kiroho.

---

[2] https://en.wikipedia.org/wiki/Isaac_Newton#Mechanics_and_gravitation
[3] Ibid

## 2. Tufaha Iliyoanguka

Nikiwa ninafanya kazi katika taasisi ya kikristo nilikuwa katika nafasi ya kushuhudia athari za dhuruma za kimapenzi. Kutazama baadhi ya kiwewe ambacho mtu huyu alipitia ilikuwa sehemu yangu ya ukuaji wa utambuzi wa kiwango cha uchungu uliokuwako katika jamii. Katika hali yangu tulivu, nilianza kuuliza ni jinsi gani Mkristo anaweza kuwa amehusika katika usaliti huo mkubwa wa imani, kwa vile baadhi ya waathiriwa hawa walikuwa wamenyanyaswa na viongozi wa kuaminika wa kanisa. Lilikuwa wazo ambalo liliingia moyoni mwangu. Ni jinsi gani mtu ambaye anaamini ndani ya Kristo na anaheshimika kama kiongozi anarusu vitu hivi kutendeka, sio kwa kiwango kidogo, lakini kwa utaratibu wa kuuguza?



Kuna tukio la karibuni ambapo nilipokea simu ya kukatiza tamaa. Nilijua nilihitaji kuenda kusaidia. Washiriki wawili wa ushirika wa Kristo niliokuwa nahudumia walikuwa katika ugomvi wa kuchukiza. Nilipofika nilisikia vurugu na nikaomba hekima na neema. Kulikuwa na hofu katika macho ya watoto wazazi walipomwagiana uchungu wao. Katika kanisa hauwezi kuwa na vidokezo vingi kuwa mgogoro kama huo ulikuwepo. Hali usiku huo ilipikika, lakini iliwasha kitu ndani yangu.

Nilikumbuka takwimu ambayo nilikuwa nimesoma awali katika mafunzo yangu kuhusiana na talaka na dhuruma za kimapenzi. Takwimu hiyo sasa ilikuwa na sura na majina kadhaa. Uzito wa hali ulionyeshwa na ukweli wa kikatili. Wakati huo ndio nilikumbuka wakati tufaha ilianguka akilini mwangu na wazo:

*Kuna kitu ambacho kinakosa. Hatuna majibu*, niliwaza. Tukio la pekee hapa na pale ningeweza kufahamu, lakini sio sura ambazo zilikuwa mbele yangu: Mmoja kati ya watoto kumi sasa ni mwathiriwa wa dhuruma za kimapenzi.[4] Katika shirika ambalo nilikuwa nikitenda kazi viwango vya talaka vilikuwa juu kama 28% na migogoro ya ndoa ilikuwa juu kama 58% katika maeneo mengine.[5]

Singeweza kupuuza takwimu hizo. Niliamua kutafuta jawabu lenye maana katika kuvunjika huku kwa familia na mahusiano ya jamii. Jambo hili lilikuwa la kutatanisha zaidi kwa sababu ya thamani ya juu ambayo watu wengi huweka juu ya Familia zao kote nyumbani na kanisani. Fikiria kauli kama zifuatazo:

> Familia ndio kitu muhimu zaidi ulimwenguni. – *Princess Diana*
>
> Nguvu za taifa hupatwa kutoka kwa uadilifu wa nyumbani. – *Confucius*
>
> Wakati wa furaha zaidi katika maisha yangu umekuwa ule mchache ambao nimepitisha nyumbani kifuani mwa familia yangu. -- *Thomas Jefferson*
>
> Tunza uhusiano wako na binadamu– mahusiano yako na marafiki na familia. – *Barbara Bush*

Kauli hizi nazisikia mara kwa mara, lakini bado kuna ugomvi, migogoro na dhuruma nyingi katika familia na jamii kwamba zinaomba swali: ni kanuni zipi za msingi ambazo zitapelekea mahusiano yenye nguvu na yenye afya? Kuna sheria ya jumla ambayo inahusiana na mwendo wa moyo ambao unaelewa kwa juu na ukifanyiwa mazoezi unaweza leta uiano katika mahusiano yetu na kupunguza ugomvi na dhuruma?

---

[4] Darkness to Light. End Sexual Abuse. www.d2l.org – figure released Aug 2013.

[5] http://family.adventist.org/home---divorce-and-remarriage-in-the-seventh-day-adventist-church.html

Kama mawazo ya Newton mawazo yangu yalivutwa kwa uhusiano wa vitu vya mbingu katika mawingu, nikitafuta mwongozo au mpangilio ambao ungeweza kuyajibu maswali katika mawazo yangu. Jitihada zangu zilinipeleka mbali zaidi na vile nilivyotarajia na kwa hivyo, kichwa cha kijitabu hiki, *Mpangilio Takatifu wa Maisha*. Katika kutafuta majibu ya kupata siri ya mahusiano yaliyofanikiwa, niliwekwa wazi kwa ukweli rahisi ambao unazungumza hekima katika masuala mengi ya uzoefu wa mwanadamu. Kama nilivyoangalia umbali ambao kanuni hii imefika, ninashangazwa na kusisimuliwa na athari. Nimefanya majaribio kadhaa ambayo yameleta matokea ya ajabu kwa msingi wa kanuni hizi.



Kama utangulizi wacha tuzingatie mtindo ambao tunapokea uzima. Baba hupitisha mbegu yake kwa mama, ambaye hulea na kukuza mtoto katika tumbo lake, kisha huzaa. Kanuni ya **utendaji wa chanzo cha uzalishaji** ya baba yetu na kanuni ya **upokeaji ya mtindo wa uleaji** ya mama inatupa umaizi kwetu kuhusiana na mpangilio wa ajabu wa uumbaji, kwa sababu hivi ndivyo sisi sote tumekuja katika ulimwengu huu. Mfungamano wenye uiano wa chanzo na mkondo unatupa maisha. Upanuzi wa kanuni hii rahisi na athari zake katika kila masuala ya maisha yetu ndio mada katika kijitabu hiki. Kama sehemu ya safari yetu pia tutagundua kanuni nyingine ambayo iko katika vita na mpangilio huu wa uzima, kanuni hasi ambayo imeleta kuchanganyikiwa na kuumbukwa kwa uiano wa mpangilio huu, na kuleta huzuni, mchafuko, na kifo.

Wacha tugeuke kwa vitu vya mbinguni ambavyo vilikuwa sehemu ya kile ambacho Newton alikuwa akiangazia kwa mtazamo halisi. Fikiria uhusiano wa jua, mwezi, na dunia tunapoangazia masuala ya nuru, mvuto (gravity) na mapigo ya mawimbi yanayohusiana na vitu hivi.

## 3. Akisimama juu ya Mwezi Akivikwa Jua





Simama juu ya mpaka wa Bonde la Minas katika Nova Scotia wakati wimbi linakuja na utasikia kinachoitwa "sauti ya mwezi", katika namna ya billioni 14 za tone ya maji yakitririka kwa bonde ambapo mawimbi makali ulimwenguni hutokea. Haijawahi fahamika hadi wakati ambao Newton alichapisha kanuni (*Principia)* ndio ulimwengu ulitambua uhusiano uliopo baina ya jua, mwezi, na mawimbi.[6] Ufahamu wa mwendo wa mawimbi ni muhimu kwa wale wanaofanya shughuli baharini kufaulu katika kuzunguka bahari. Faida ya kujua athari za mvuto za mwezi haikuwasaidia tu mabaharia kwa wakati uliopita. Nilijifunza hivi karibuni kutoka kwa kwa rafiki wa zamani kwa mawimbi bora huja wakati wa mwezi mpya na mwezi mzima. Matukio haya yanajulikana kama mawimbi ya chemchemi (spring tide).

> Wakati mwezi ni mzima au mpya, msukumo wa mvuto wa mwezi na jua huunganika. Na nyakati hizi, mawimbi marefu huwa ni marefu sana na mawimbi mafupi ni mafupi sana. Hili linajulikana kama mawimbi marefu ya chemchemi (spring high tide). Mawimbi ya chemchemi hasa ni mawimbi yenye nguvu (hayahusiani kwa vyovyote na msimu wa chemchemi). **Hutokea wakati Nchi, Jua, na Mwezi viko katika mstari. Nguvu za mvuto (gravitational forces) za Mwezi na Jua zote huchangia kuwepo kwa mawimbi.** Mawimbi ya chemchemi hutokea wakati wa mwezi mzima na mwezi mpya.[7]

Wakati jua, mwezi, na nchi zimefungamana huwa zinaleta nguvu zaidi ya mvuto juu ya nchi ambayo hutoa mawimbi makuu, bila shaka, mawimbi marefu. Ingawaje mvuto wa jua ni mkubwa zaidi kuliko ule wa mwezi,

[6] http://www.thehighesttides.com/what-causes-the-highest-tides.shtml
[7] http://home.hiwaay.net/~krcool/Astro/moon/moontides/

ukaribu wa mwezi kwa nchi hufanya athari zake za mvuto juu ya nchi kuwa mara mbili zaidi ya zile za jua. Muhimu kwa mawimbi ya chemchemi ni mkao wa jua, mwezi, na nchi.




Takriban wiki mbili za mfuatano wa mwendo wa mawimbi unaathari kubwa juu ya mawimbi na viumbe wa baharini. Kama ungekuwa ukiogelea katika "Great Barrier Reef" kuelekea pwani ya kaskazini mwa Queensland katika Australia wiki nne hadi sita baada ya moja ya mwezi mzima katika mwaka, unaweza shuhudia tukio kubwa la uzalishaji mwingi katika sayari. Matimbawe huzaa wakati mawimbi yametulia (hakuna mwendo wa mawimbi kwa upande wowote), kama ilivyo kinyume aina nyingi za samaki ambao hunufaika na mawimbi makubwa kwa kuosha mayai yao katika usalama hasa wa maji wazi.[8]

Lakini mzunguko wa mwezi pia huathiri kipindi cha ujauzito wa wanyama kama vile wenye uti wa mgongo, na mzunguko wa hedhi wa wanawake ni karibu sawa na mzunguko wa jua.[9] Hivyo basi kuna ushahidi kuonyesha kuwa kuna uhusiano kiasi kati ya uwezo wa kuzaa na uzazi na mzunguko wa mwezi.


Tunaweza jifunza kitu kutoka kwa mfuatano wa mawimbi ya maumbile? Uhusiano wa jua na mwezi kwa nchi unaweza kuwa kiambato muhimu cha kutambua siri kwa mahusiano yetu ya kiroho? Kama mafanikio na uwezo wa kuzaa wa maisha halisi yana chanzo chake maarifa ya mfuatano wa mwendo

---

[8] http://www.greatbarrierreefs.com.au/coral-spawning/
[9] https://en.wikipedia.org/wiki/Tide#Biological_rhythms

wa mzunguko wa jua na mwezi kwa uhusiano na nchi kunaweza kuwa na somo la kujifunza katika kiwango cha kiroho?

Kabla ya kupiga hatua katika upande huo, wacha tuangazie uhusiano mwingine wa kuvutia kuhusiana na jua, mwezi, na nchi. Mwezi hauna nuru yake. Ni kitu kisichokuwa. Nuru yote ya mwezi ni mwakisi wa mwanga kutoka kwa jua. Jua hujizalishia mwanga wake; ina kanuni ya utendaji. Jua la utendaji na mwezi usiokuwa katika utendaji hufanya kazi pamoja ili kuunda athari za mfuatano wa mwendo juu ya nchi. Tena, kuna mafunzo hapa ya uhusiano wa jua na mwezi ambayo hutuzungumzia kuhusu mfuatano wa mwendo wa maisha katika ulimwengu wa kiroho?




Fikiria kile ambacho hutendeka unapojaribu kuangalia jua moja kwa moja. Mwangaza wa jua hufanya isiwezekane kulitazama kwa zaidi ya sekunde chache. Kuliangalia jua kutaharibu uwezo wako wa kuona. Kuna njia yoyote ya kuangalia jua? Ndio, tunaweza tazama mwanga wa jua kwa kuangalia mwezi moja kwa moja, na hivyo basi kuondoa hatari ya kuharibika macho yetu. Mwangaza unaotolewa kwa jua hupitishwa kupitia kwa mwezi, hutenda kama mjumbe wa kupitisha mwanga kwetu kwa usalama na bila madhara yoyote. Swali ambalo linaomba kuulizwa ni, “Kuna maana kwa hili?” uwepo wa kuamuru wa jua ni kijenzi muhimu katika uzima wote. Miale yake hutuletea joto na mwanga, na hutenda jukumu la muhimu sana katika uwezo wa kuzaa wa sayari, lakini tusipoliheshimu jua linaweza tuletea madhara. Tena, kuna mambo hapa kwetu ya kujifunza?

Mwonaji wa kale Yohana akiwa ameketi katika kisiwa cha Patimo katika bahari ya Mediterrania, aliona ajabu kuu katika maono:




Kukaonekana ishara kuu mbinguni: Palikuwa na mwanamke aliyevikwa jua na mwezi ukiwa chini ya miguu yake na taji ya nyota kumi na mbili ilikuwa kichwani mwake: Ufu 12:1

Yohana anaelezea uhusiano kati ya jua, mwezi, nyota na mwanamke. Amesimama juu ya mwezi. Huu ndio msingi wake. Amevikwa mwanga wa jua na ana mwanga wa nyota kumi na mbili juu ya kichwa chake. Anaonekana kuwa na uiano mkamilifu na mzunguko na majira ya jua, mwezi, na nyota na anatambua uhusiano wake navyo. Tukijua kuwa kitabu cha Ufunuo kilikuwa kitabu chenye maudhui ya kiroho, hakitaweza kuwa na umuhimu wa kiroho?

Kabla ya kujibu hili tunahitaji kuuliza, “Tunaweza kuamini maandiko ya Bibilia kama muongozo wa kuaminika katika vitu vya kiroho?”

# 4. Ramani na Dira ya Kiroho



Gavana wa Kirumi Pilato alikuwa amezoea nyuso za watu wengi waliokuwa wakisimama mbele yake katika hukumu ndani ya chumba chake cha hukumu katika Judea. Kulikuwa na kitu tofauti kabisa katika uso wa mtu huyu. Nje, kulikuwa na mkutano uliokuwa ukipigia yowe kifo cha mtu, lakini bado hakukuwa na hofu usoni mwake. Pilato alikuwa na ufahamu wa mhalifu mgumu, na mtu aliyekuwa akisimama mbele yake kwa hakika hakuwa mmoja wao. Gololi ya cheo chake na kutazama kwa upole na ungwana kulifitini hakimu. Alinena kuhusu ufalme zaidi ya ulimwengu huu—ufalme ambao ulikuwa zaidi ya siasa, ushindi na vita. Alikuwa ameshtakiwa kwa kupanga njama dhidi ya serikali ya Roma chini ya cheo cha Masihi wa Wayahudi aliyetarajiwa kwa muda mrefu.

> Pilato akamwuliza, "Kwa hiyo Wewe ni mfalme?" Yesu akajibu, "Wewe wasema kwamba mimi ni mfalme. Kwa kusudi hili nilizaliwa na kwa ajili ya hili nilikuja ulimwenguni ili niishuhudie kweli. Mtu ye yote aliye wa kweli husikia sauti yangu." Yohana 18:37

Mfalme ashuhudiaye kweli? Ni mfalme yupi aliwahi shuhudia kweli? Wafalme kwa kawaida walishinda na kuhifadhi uongozi wao kwa vita, udanganyifu, kutoa hongo, na kutumia nguvu. Kisha Pilato akauliza swali muhimu sana. "Kweli ni nini?" kuweka hili kwa njia nyingine, mtu anaweza uliza, "Tunawezaje ijua kweli?"

Kila mtu mwenye kufikiria ana chanzo cha mamlaka, chumba cha kweli, pahali au mtu ambapo wanaujasiri kuwa wanapata ujumbe sawa kuhusiana na uhalisia wa uzima na kifo. Kwa watu wengi chanzo hiki ni akili zao wenyewe. Kile ambacho wanaona, kusikia, kushuhudia, na kusoma kinatosha kwao kuamua kweli. Wanaujasiri kwamba lenzi ambayo kwayo wanaona ulimwengu haijaumbuka kwa njia yoyote.

Ukumbusho japo kwa kifupi wa jinsi watoto hujibu swali la uchunguzi kwa wazazi wao wakati wamekanyaga nje ya mipaka ya kanuni za familia unapaswa kututhibitishia kuwa tuna mwelekeo asili wa kukunja na kufurukuta ukweli ili ufae hali yetu. Mfano mwingine ambao tunaweza angazia ni jinsi wanasiasa wengi hujibu maswali kutoka kwa vyombo vya habari kwa namna ambayo huepuka kutiwa katika swali. Tunaweza jitegemea kugudua ukweli kama tuna mazoea ya kuukunja na kuuepuka wakati ambao hautufai?

Kuna wale katika kundi lingine wanaamini tu katika utamaduni uliopitishwa kwao kutoka kwa mababu zao. Tunawezaje jiamini au kuamini mababu zetu kwa ukweli huru na kamili? Kama tunajua kwamba sisi wenyewe tunakabiliwa na mazoea ya kupotosha ujumbe, je, Hilo linaweza kuwa limefanywa na wale waliotutangulia?

Pamoja na mazoea ya binadamu ya uongo, kudanganya, kutia chumvi au kupuuza, tunawezaje kupata kweli? Hili linaturejesha kwa swali la Pilato, "Kweli ni nini?" mbele yake alisimama mtu ambaye aliruhusu ajaribiwe kikamilifu katika hatua hii. Alisema kuwa alikuja ashuhudie kweli, na ni madai yake kuwa yeye ni Masihi ndiyo yalifanya rahisi kwake kijaribiwa.

> Akawauliza, "Je, ninyi, mnasema mimi ni nani?" (16) Simoni Petro akamjibu, "Wewe ndiwe Kristo a, Mwana wa Mungu aliye hai." (17) Naye Yesu akamwambia, "Heri wewe, Simoni mwana wa Yona, kwa maana hili halikufunuliwa kwako na mwanadamu, bali na Baba yangu aliye mbinguni. Mathayo 16:15-17

Kwa kuweka madai kuwa yeye ni Masihi, Yesu alikuwa anajiweka kuwa mada ya unabii wa Agano la Kale kuhusu Masihi. Unabii huu wote ulikuwa umeandikwa mamia ya miaka kabla ya wakati wa Yesu.

Angazia unabii mchache kuhusu kuzaliwa kwake.

> Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda, Wala mfanya sheria kati ya miguu yake, Hata atakapokuja
>
> Yeye, mwenye milki, Ambaye mataifa watamtii. Mwanzo 49:10

Hili lilitabiri kwamba Masihi angetoka katika kabila la Yuda.

> Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele. Mika 5:2

Pia linatwambia kwamba Masihi atazaliwa Bethlehemu. Kulikuwa na mahali pawili palipoitwa Bethlehemu katika Israeli na linatambulisha pahali kama Bethlehemu Efrata.

Unabii ufuatao ni wakupendeza sana kwa kuwa unatabiri wakati ambao Masihi angekuja. Ni kwa unabii huu ndio majasusi kutoka mashariki waliweza kujua kuja na kusujudia kuzaliwa kwa Masihi.

> Basi ujue na kufahamu, ya kuwa tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. (26) Na baada ya yale majuma sitini na mawili, masihi atakatiliwa mbali, naye atakuwa hana kitu… (27) Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu. Danieli 9:25-27

Haya ni machache ya mafungu mengi, mengi ya unabii kuhusu Masihi. Ukifanya utafiti kiasi wa jinsi mtu Yesu Kristo alitimiza unabii wote utagundua usahihi wa ajabu wa Maandiko. Mwandishi mmoja alikokotoa uwezekano wa 48 ya unabii huu kuweza kutimizwa kwa mtu.[10] Matokeo yalikuwa 1 katika $10^{157}$. Hiyo ni 1 katika

10,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,
000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,
000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,000,
000,000,000,000

[10] Evidence that Demands a verdict, Josh McDowell (1972) p.167



Kwa ulinganishi, $10^{137}$ ni makadirio ya hesabu ya protoni katika ulimwengu. Mfano mwingine utakuwa kama kujaribu kutafuta nafaka moja ya mchanga kutoka kwa mchanga wote ambao unapatikana duniani na hata zaidi kabisa. Fikiria kile $10^{17}$ tu inaweza husisha. Hili lote, hesabu ndogo zaidi inaweza kuwa kama kuzunguka nchi ya Ufaransa kina cha 60cm kwa sarafu za Euro 1. Moja weka alama ya x, changanya sarufu na kisha mtume mtu mmoja bila kujua akaitafute sarufu hiyo moja—kwa jaribio la kwanza. Uwezekano unatisha, na huu tu ndio unabii unaohusiana na Masihi.

Kuna unabii mwingine unaohusiana na kuinuka na kuanguka kwa falme za ulimwengu katika kitabu cha Danieli ambao umetimia kwa usahihi. Wengine wameamua kuwa haiwezekani unabii huu kuwa kweli wamehitimisha kuwa lazima uliandikwa baada ya matukio.



Vitabu vya bahari ya kifo, viligunduliwa baada ya 1946 vilikuwa na mengi ya Agano la Kale na vinawekewa tarehe angalau karne ya tatu kabla ya Kristo. Vinathibitisha kuwa unabii ulifanywa angalau miaka mia mbili kabla ya kuja kwa Yesu. Hakuna mtu mwingine katika historia ambaye ameungwa mkono na kwa kiwango kama hiki cha usahihi, kitabu kingine kinaweza dai kiwango cha maelezo katika kutabiri siku za baadaye kama Bibilia. Aina hii ya usahihi ni vigumu kupunguzwa, isipokuwa, bila shaka, tukimbilie tabia ya wanasiasa ya kupotosha ukweli kwa sababu hautufai. Nakwalika ujaribu

usahihi wa Bibilia kupitia kwa unabii wake, hasa ule ambao unahusiana na utu wa Yesu. Kama unaweza kufikia YouTube tazama wasilisho, "Bible Prophecy of Jesus. Just another Man?" na Dr Walter Veith.[11]

Kuweka maana katika usahihi wa unabii kuhusu Masihi kunapendekeza kuwa mambo ambayo anatwambia, na mambo yanayosemwa kumhusu katika Bibilia, yanastahili uangalifu wa karibu. Tukiwa na kanuni ya chanzo na mkondo ambao tumegundua kwa umbali huu, wacha sasa tuangalie katika Bibilia ili tuone jinsi inatuelezea Mpangilio huu wa Maisha.

[11] https://www.youtube.com/watch?v=gdXbT5cII7U

## 5. Mpangilio Takatifu

Pilato alikuwa ameuliza swali muhimu kwa Yesu. “Ukweli ni nini?” kama angesubiri jibu angepokea maneno haya. “Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu.” Yohana 14:6. Yesu anaeleza ukweli kwa njia ya uhusiano wake kwa Baba. Yeye ndiye njia ya kwenda kwa Baba. Katika mahali pengine alipokuwa akizungumza na wafuasi wake Yesu aliwauliza wanafunzi,

> ...“Je, ninyi, mnasema mimi ni nani?” (16) Simoni Petro akamjibu, “Wewe ndiwe Kristo a, Mwana wa Mungu aliye hai.” (17) Naye Yesu akamwambia, “Heri wewe, Simoni mwana wa Yona, kwa maana hili halikufunuliwa kwako na mwanadamu, bali na Baba yangu aliye mbinguni. Mathayo 16:15-17

Jibu kwa swali la Pilato lilikuwa kuwa Yesu ndiye kweli, na hoja ya msingi katika ukweli huu ni kuwa Yesu ndiye mkondo au njia ya kwenda kwa Baba. Huu ndio ukweli wa Mpangilio takatifu, na Paulo katika waraka wa kwanza kwa Wakorintho anaelezea Mpangilio huu kwetu.

> Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, **ambaye** vitu vyote vyatoka Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye **kwa Yeye** vitu vyote vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi. 1 Wakorintho 8:6

Mpangilio unagunduliwa katika maneno mawili ambayo yanafuata, majina ya Baba na Yesu Kristo.

| Kuwa | Mpangilio | Maelezo (Kutoka kwa Rejeshi ya Strong) |
|---|---|---|
| Baba | ἐκ<br>Ambaye | ek, ex – Kiunganishi cha msingi kinachoonyesha *asili, chanzo* (mahali ambapo mwendo au tendo hutoka) |
| Yesu Kristo | δια<br>Kwa yeye | dia *dee-ah'* - Kiunganishi cha msingi kinachoonyesha *njia/mkondo* wa tendo; *kupitia*. |

Jiwe la pembeni la uhusiano wa ulimwengu ni ἐκ→ δια au kwa Kiswahili, Ambaye na Kwa Yeye. Baba ni *mwanzilishi* wa nini? “Vitu vyote.” Yesu Kristo ni *mkondo au njia* ya nini? “Vitu vyote.” Hapa tunapata kanuni ya mahusiano ya jumla ikiwemo uzima wenyewe. Tunaweza ieleza kwa njia hii, wapi ζωη zoe ni jina la Kiyunani la uzima:

ἐκ → δια = ζωη

Chanzo → Njia/mkondo = Uzima



Kumbuka tena mfano wetu wa jinsi wanadamu hupokea uzima. (ἐκ, chanzo) hupitisha mbegu yake kwa mama (δια, njia), na uzima hutolewa. Hii ndio siri ya asili ya aina zinazotajwa katika Mwanzo.

> Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. Mwanzo 2:21, 22

Kuna uhusiano upi kati ya Adamu na Hawa? ἐκ → δια. Chanzo cha aina kilikuwa katika Adamu. (Ambaye). Kwake malighafi yenye uzima yalitolewa ili kuunda njia ya aina, mwanamke (kwa yeye). Na kwa hivyo kila mtu anayezaliwa katika ulimwengu huu anahitaji ἐκ → δια (chanzo-njia) mfumo wa kupokea uzima. Adamu alifahamu hili aliposema,

> Adamu akasema, Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana **ametwaliwa katika mwanamume**. Mwanzo 2:23

Kupitia kwa msaada wa maneno yaliyovuviwa ya Maandiko tunaweza kutazama uhusiano wa kiroho wa watu wa mbingu Baba na Mwana. Katika kuangalia uhusiano huo tunagundua sheria ya jumla ya viumbe vyote ambayo ni ἐκ → δια, chanzo-njia. Angazia pia mafungu machache zaidi ya Maandiko.

> Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu... Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mwanzo 1:26, 27
>
> Kuweka wazi kwa kila mtu jinsi ile siri iliyokuwa imefichwa kwa nyakati zote katika Mungu aliyeumba vitu vyote **kupitia** Yesu Kristo; Waefeso 3:9
>
> Vitu vyote viliumbwa **kwa Yeye**, wala pasipo Yeye hakuna cho chote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa. (4) Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu. Yohana 1:3-4

Mungu aliumba vitu vyote kupitia kwa Yesu Kristo. Ilikuwa kwa Mwanawe ambapo Mungu alisema "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu." Sura ya

mahusiano ambayo kwayo aina ya mwanadamu iliumbwa ilikuwa uhusiano wa Baba na Mwana, na uhusiano huo ni ἐκ → δια, Chanzo-Njia.

> Kwa maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu, asili ya Mungu asiyeonekana kwa macho, yaani, uwezo Wake wa milele na asili Yake ya Uungu, umeonekana waziwazi ukitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya ili wanadamu wasiwe na udhuru... Warumi 1:20

Kitabu cha Warumi kinatwambia kuwa sifa zisizoonekana za Uungu zinaonekana wazi kwa vitu ambavyo vimeumbwa. Ni nini hasa kiliumbwa kwa sura haswa ya Mungu? Mwanamume na Mwanamke na uhusiaano wanaodumisha kwa kila mmoja wao. Uhusiano wa binadamu wa mme na mke umeundwa katika mpangilio wa Baba na Mwana ambaye anaunda uhusiano wa msingi wa Ulimwengu.

Tukiwa na mawazo haya akilini wacha tuangazie mafungu zaidi machache kutoka kwa Bibilia.

> ...kuwa watiwe moyo na kuunganishwa katika upendo, ili wapate kujua ulivyo utajiri wa ufahamu kamili, waijue siri ya Mungu, yaani, Kristo mwenyewe, (3) ambaye ndani Yake kumefichwa hazina yote ya hekima na maarifa. Wakolosai 2:2-3

Uhusiano wa Baba na Mwana ni sahihi takatifu ambayo iliwekwa juu ya uumbaji. Kama ukiangalia angani utaona sahihi hii juu ya jua na mwezi. Unapoangalia asili ya aina utapata sahihi hii takatifu. Tukiwa na ufunguo huu takatifu tunaweza fungua hazina ya hekima na maarifa.

> Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho. 2 Wakorintho 3:18

Kwa kutazama sahihi hii takatifu ya ἐκ → δια, Chanzo-Njia, katika Baba na Mwana, mawazo yetu, hisia, mahusiano yetu, na utafiti wetu utabadilishwa na mpangilio huu. Naipata erevu kabisa kuwa siri kwa hekima na maarifa yote kwa imara kweli imeunganishwa na maarifa ya mahusiano ya Baba na Mwana. Ufahamu usiokuwa sahihi wa uhusiano wao bila shaka utaharibu ufunguo na huchujuka maarifa na hekima ya kweli. Hata hivyo, tukiwa na maarifa haya ya kweli na kuendelea kutafakari juu ya Baba na Mwana, mpangilio huu huanza kudhihirishwa katika fahamu na kuleta uiano katika akili na mioyo yetu na kwa akili na mioyo ya wale ambao tunahusiana nao.

Jedwali 1 – Chanzo cha Kanuni

| Kifungu | | Asili (Baba) - ἐκ → | Njia (Mwana) - δια |
|---|---|---|---|
| Yeye ni **mfano** wa Mungu **asiyeonekana**, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Wakolosai 1:15 | 1 | Asiyeonekana | Anaonekana |
| Mwana ni **mng'ao** wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake … Jina **alilorithi** lilivyo bora kuliko lao… Waebrania 1:3, 4 Kwa hiyo, **Mungu alimtukuza sana na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina… kwa utukufu wa Mungu** Baba. Wafilipi 2:9-11 | 2 | Utukufu | Mng'ao (mtukuza) |
| Mwana hawezi kufanya jambo lo lote peke yake, Yeye aweza tu kufanya lile analomwona Baba yake akifanya, Yohana 5:19. Lakini napenda mfahamu kwamba kichwa cha Kristo ni Mungu…**kichwa cha Kristo ni Mungu.** 1 Wakorintho 11:3 | 3 | Uongozi | Utiifu |
| Je, ni kwa malaika yupi ambaye Mungu amepata kumwambia wakati wo wote, "W**ewe keti** mkono Wangu wa kuume mpaka **nitakapowaweka** adui Zako chini ya nyayo Zako?" Waebrania 1:13, Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu Atakaa katika uvuli wake Mwenyezi. Zaburi 91:1 | 4 | Mlinzi | Mlindwa |
| Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye." Mathayo 3:17 Lakini Yesu akajibu, "Imeandikwa, 'Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.' '' Mathayo 4:4 | 5 | Mtoaji wa mibaraka/ Mpaji | Mpokeaji wa mibaraka |
| Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu. Isa 57:15, Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu… Yohana 1:14 | 6 | Aliyetukuka (Ukaribu wa mbali) | Uhusiano wa Karibu (Ukaribu sana) |
| Mimi **nimekuja kwa Jina la Baba Yangu**, nanyi hamnipokei, lakini mtu mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea. Yohana 5:43 | 7 | Mwakilishwa (Wazo) | Mwakilishi (Neno) |

Kuna kanuni kadhaa zinadhihirishwa hapo juu kwa kutazama tu tabia ya Baba na uhusiano wa Mwana. Tutapanua kanuni hizi katika sura zijazo.

Jedwali 2 – Mifano ya Njia/Mkondo

| Chanzo – ἐκ → | Njia – δια | |
|---|---|---|
| Mume | Mke | Kichwa cha **mwanamke** ni **mwanaume**. 1 Kor 11:3 |
| Mzazi | Mtoto | Waheshimu **baba yako** na **mama yako**. Matt 19:19 |
| Kristo | Kanisa | Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe kama vile **Kristo** alivyo kichwa cha **Kanisa**; Efe 5:23 |
| mchungaji | Kundi | **Lichungeni kundi** la Mungu mlilokabidhiwa, mkitumika kama waangalizi. 1 Pet 5:2 |
| Kiongozi | Wananchi | **Kila mtu na atii mamlaka inayotawala**, kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu, nazo mamlaka zilizopo zimewekwa na Mungu. Warumi 13:1 |
| Fikira | Hisia | Jaribuni kila kitu. Yashikeni yaliyo mema. 1 Wathess 5:21 |
| Imani | Matendo | …**imani itendayo kazi** kwa njia ya upendo. Wagalatia 5:6 |
| Kristo | Bibilia | Naye akianzia na **Musa na manabii wote**, akawafafanulia jinsi maandiko yalivyosema **kumhusu Yeye**. Luka 24:27<br>Ninyi mnachunguza Maandiko mkidhani ya kuwa ndani yake mna uzima wa milele, maandiko haya ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yohana 5:39 |
| Agano la Kale | Agano Jipya | “Msidhani kwamba nimekuja kuondoa **Torati au Manabii**, sikuja kuondoa bali **kutimiza**. Matt 5:17 |
| Sheria 4 za kwanza | Sheria 6 za mwisho | Yesu akamjibu, “‘Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa roho yako yote na kwa akili zako zote.’ (38) Hii ndio amri iliyo kuu, tena ni ya **kwanza**. (39) Nayo ya **pili** ni kama hiyo, nayo ni hii: ‘Mpende jirani yako kama nafsi yako. Matt 22:37-39 (RV) |
| Mbegu | mmea/Mti | Luka 8:5-8 "Mpanzi alitoka kwenda kusia **mbegu**… (8) Mbegu nyingine zilianguka penye udongo mzuri. Zikaota na **kuzaa** mara mia zaidi ya mbegu alizopanda." |
| Jua | Mwezi | Mungu akafanya mianga miwili mikubwa, ule **mkubwa** utawale mchana, na ule **mdogo** utawale usiku. Mwanz 1:16 |

Jedwali la pili ambalo limeonyeshwa hapo juu ni sura ya jedwali la kwanza. Zote ziko katika ἐκ → δια, chanzo-njia, uhusiano.

Vipengele vingi vya sahihi takatifu vinaweza onekana vikitenda kazi katika ulimwengu wetu. Nafasi ya asili na njia hubadilika kutegemea uhusiano. Kwa mfano, katika uhusiano wa mume na mke mume ndiye asili, na mke ndiye njia. Katika uhusiano wa mama na mtoto mama ndiye asili, na mwana ni njia.

Tunapochukua kanuni ya Mpagilio Takatifu ulioelezewa katika jedwali la kwanza na kuzitumia kwa uhusiano unaoelezewa katika jedwali la pili, tunagundua siri ya mwendo wenye uiano wa vitu vya duniani katika tamasha na vitu takatifu vya mbinguni vya ulimwengu—Baba na Mwana.

Ni muhimu kukumbuka kuwa katika mfano wa chanzo unaotolewa katika jedwali la pili, mamlaka yao hatimaye yananyenyekeshwa kwa Mungu ambaye aliyatoa. Hakuna mamlaka yoyote ulimwenguni ambayo yanajitegemea kikamilifu, na maombi yoyote yanayotolewa ya njia husika lazima yawe na uiano hatimaye na mamlaka ya Mungu. Kama hayako katika uiano sio tu haki bali pia wajibu wa yule anayeimiliki njia kwa heshima kukata rufaa kwa mamlaka ya juu.


Kufupisha kanuni hizi ambazo tumetaja:

1. Asiyeonekana na anaonekana:
   Njia inadhihirisha au ni njia ya kuenda kwa chanzo.
2. Utukufu na Mng'ao: njia inatukuza chanzo.
3. Uongozi na Utiifu: njia inatii chanzo.
4. Chanzo hulinda njia.
5. Chanzo hubariki njia.
6. Chanzo hutoa kwa njia.
7. Chanzo huwakilishwa na njia.

Orodha yetu inaanza na matendo ya njia kwa sababu inatuongoza kwa chanzo, sawasawa na Kristo anavyotuongoza kwa Baba. Pindi tunapounganishwa kwa chanzo, basi tunaweza kudhihirisha matendo yake.

Kanuni ambazo tumeelezea zinatupa kokwa ya mpangilio takatifu. Kuthamini kwa kweli urembo na ulinganifu wa mpangilio huu, lazima kiasili tutoe ukuzaji wa hili katika mfano wa sura inayotolewa katika jedwali la pili.





Mke na mume

Wazazi na Watoto


Kristo na Kanisa




Mbegu na mti

Jua na Mwezi

## 6. Kijito cha Uzima



Ili kukamilisha utangulizi wetu kwa mpangilio takatifu tunahitaji tu kuuliza swali, “Chanzo na njia ya *nini*? Wacha tureje kwa fungu kuu la Bibilia:

> Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, **ambaye vitu vyote vyatoka** Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, **ambaye kwa Yeye vitu vyote** vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi. 1 Wakorintho 8:6

Jibu tu ni *vitu vyote*. Hivyo ni nini kinajumuishwa katika *vitu vyote*?

> Kisha yule malaika akanionyesha mto wa maji ya uzima, maangavu kama kioo yakitiririka kutoka kwenye kile kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo. Ufunuo 22:1

Mwana-kondoo katika fungu hili anarejelea Mwana wa Mungu (Yohana 1:29). Uzima wote hutoka kwa Baba na hupitishwa kupitia kwa Mwana. Baba ni chanzo cha uzima na Mwana ni njia ya uzima. Uzima huu hutiririka kwetu kupitia kwa Roho wa Mungu. Roho mara nyingi hurejerewa kama mwanga, maji, upepo na pia moto katika Bibilia. Ni kwa Roho wa Mungu kwamba

tunashuhududia utimilifu wote wa mibaraka ya Mungu. Mahali tu ambapo tunaweza pokea Roho huyu ni kupitia kwa njia– Mwana wa Mungu.

> Yesu akawaambia tena, "Amani iwe nanyi! Kama vile Baba alivyonituma Mimi, Mimi nami nawatuma ninyi." (22) Naye alipokwisha kusema haya, akawavuvia, akawaambia, "Pokeeni Roho Mtakatifu." Yohana 20:21-22

Katika wakati wa sasa ulimwengu wote hupokea uzima juu ya nchi kwa sababu ya Karama ya Yesu msalabani. Wale ambao hukataa kukubali mahali ambapo uzima huu hutoka hatimaye watajitenga kutoka kwa chanzo. ili kupokea uzima huu milele tunahitaji kutambua mfungamano wa chanzo na njia wa Baba na Mwana.

> Huu ndio ushuhuda kwamba, Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe. (12) Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima. 1 Yohana 5:11-12

Uzima ni wa kwanza katika mibaraka mingi ambayo humwagwa juu yetu. Hapa kuna lingine:

> Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16

> Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha upendo Wake kwetu, kwa sababu Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye. 1 Yohana 4:9

Upendo hupata chanzo chake katika moyo wa Baba na kudhihirishwa kwetu kupitia kwa njia ya Mwanawe. Hivyo upendo ni kijito kitiririkacho kutoka kwa chanzo na kuendelea na kupitia kwa mkondo/njia. Kijito cha upendo kinaweza onyeshwa kwa namna mbalimbali katika mpangilio.

| Chanzo – ἐκ → (Haonekani) | Channel – δια (Anaonekana) | Kijito/Uzima - ζωη |
|---|---|---|
| Wazo | Neno | Upendo |
| Wazo | Kukumbatia | Upendo |
| Wazo | Karama | Upendo |

Mawazo ya upendo ambayo kamwe hayadhihirishwi au kuonyeshwa kamwe hayajulikani kuwepo, na kama kamwe hayajulikani hayawezi pokelewa na kushuhudiwa. Njia ya Mwana wa Mungu ni muhimu jinsi gani katika Mpangilio Takatifu ili kujua moyo wa Baba!

Tukirejea kwa mfano wa jua na mwezi tunagundua kanuni nyingine muhimu. Kama tukifikiria dhana ya nuru ya maarifa ya kuja katika mawazo ya giza, kutazama jua moja kwa moja, hasa kutoka kwa hali ya giza kama hiyo, kutasababisha upofu, lakini mwanga uo huo ukipokelewa kupitia kwa ushirika wa mwezi utaruhusu mwanga ukumbatiwe bila kuleta madhara yoyote.

| Chanzo – ἐκ → (Haionekani) | Njia – δια (Inaonekana) | Kijito/Uzima - ζωη |
|---|---|---|
| Jua | Mwezi | Mwanga |
| Mzazi | Mtoto | Maarifa |

Mwanga halisi unapotujia kupitia kwa mpangilio takatifu, hivyo maarifa ya ulimwengu wetu huja kwetu kwa maelekezo. Ili tuweze kujifunza wazazi au walimu lazima watuelekeze. Tunaweza chagua kujisomea, lakini lazima tufunzwe jinsi ya kusoma na tuwe na mfichuo kwa vitabu ambavyo vimeandikwa na watu wengine. Maarifa na hekima lazima zisomwe kupitia kwa mtiririko wa maelezo. Hatuzaliwi na maarifa ya papo ya ulimwengu na mazingira yetu; huwatunajifunza kutoka kwa mwalimu au mshauri. Hapa kuna mifano zaidi ya kuangazia.


| Chanzo – ἐκ → (Haonekani) | Channel – δια (Anaonekana) | Kijito/Uzima - ζωη |
|---|---|---|
| Mzazi | Mtoto | Uzima, Upendo,Baraka, Ulinzi, Chakula, Huruma, Maarifa, Uthibitisho, Marekebisho, Mpango |
| Mwalimu | Wanafunzi | Maarifa, Uthibitisho/Baraka, Marekebisho, mpango |
| Kristo | Kanisa | Uzima, Upendo, Neema, Rehema, Baraka, Maarifa, Marekebisho, Mpango |
| Mchungaji | Kundi | Upendo, Baraka, Maarifa, Ulinzi, Marekebisho, Maagizo |
| Kiongozi | Wananchi | Maarifa, Ulinzi, Uthibitisho, Maagizo |

Hivyo Mpangilio Takatifu uko na:

1. Chanzo
2. Njia
3. Kijito

Kupitia mfungamano sahihi wa chanzo na njia, kijito kitaanza kutiririka na kuleta uzima, baraka, uwezo wa kuzaa, na mafanikio. Lakini wakati hayajafungamana na kueleweka vizuri basi tunaonja laana, uozo, na hatimaye mauti.

# 7. "Mungu wa Ulimwengu huu" Na Kuzaliwa kwa Nguvu Pinzani



Kama ungetembea katika nyumba za serikali ya mataifa mengi yanayotawaliwa na demokrasia ungepata mkusanyiko wa wawakilishi ambao wamejifungamanisha na serikali na kwa wakati uo huo wawakilishi ambao wanaweza wekwa kama wapinzani. Siku baada ya siku nguvu hizi pinzani hujadili masuala mazito ya taifa. Kila mzungumzaji hujaribu kushawishi chumba kuhusu wema wa hoja yake. Inajulikana kama *Dialectic* katika kiyunani, ilifanywa maarufu na Plato katika mazungumzo ya Socrate na ni aina ya mawazo yanayotawala ulimwenguni leo.[12] Ingawa nguvu hivi zilipinzana kwa kuonekana, kwa kweli zinafahamika kuwa zinasaidiana, na awali kile kinachotoka kwa mgogoro kinaeleweka kutoa ukweli wa hali ya juu na bora kwa wale wanaohusika na wale wanaowawakilisha.

Tukizingatia kanuni hii kwa mtazamo wa mashariki, tunapata falsafa ya China ya Yin na Yang, ambapo inatambuliwa kinyume kama giza na nuru, moto na maji, kiume na kike hakika husaidiana na hutenda kuleta uiano na usawa.[13] Kanuni hizi zimefanywa mashuhuri kupitia kwa mfululizo wa filamu ya "*Star Wars"* iliyoonyesha nguvu za nuru na giza zikitenda kinyume cha kila moja lakini mwishowe zikaleta usawa kwa *nguvu.*

Tunaelezea jinsi gani ulimwengu huu dhahiri wa kinyume; ulimwengu wa mvutano ambao upo kwa uwazi ndani yake na unatuzunguko kote? Kama tukiruhusu fikira zetu pekee zituongoze, kunaonekana kuwa na ushahidi mwingi wa uungaji mkono mitazamo kama hio. Kuazima maneno ya utangulizi kutoka kwa mfululizo wa *"Star Wars"* tunaweza sema, "Hapo zamani za kale katika nyota ya mbali, mbali kabisa."
Tukigeuka tena kwa manabii wa kale, tunaweza gundua mwanzo wa mfumo huu pinzani.

> Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! (13)


---

[12] https://en.wikipedia.org/wiki/Dialectic
[13] https://en.wikipedia.org/wiki/Yin_and_yang

Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. (14) Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye. Isaya 14:12-14

Lusifa aliumba akiwa malaika wa kupendaza na alikuwa wa kwanza miongoni mwa malaika. Aliletwa katika ulimwengu uliokuwa ukitenda kazi kulingana na kanuni ya ἐκ → δια =ζωη, chanzo-njia-uzima. Kulikuwa na uiano mkamilifu kwamba kiumbe huyo alisongelea chanzo kuu cha vyote kupitia kwa mfano mkuu wa δια – Mwana wa Baba. Uiano wa kuvutia uliokuwepo kati ya Baba na Mwana uligawiwa wenyeji wa ulimwengu kadri walivyo kumbatia mfano wa Mwana wa Mungu kama jiwe la pembeni la utambulisho wao binafsi. Kunaweza kuwa na ἐκ→ moja ya kweli, Chanzo kimoja cha mwisho cha vitu vyote, na huyu ni Baba. Uiano wa ulimwengu utambuzi wa daima wa ukweli huu. “Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.” Kumbukumbu 6:4.

Lusifa alikuja kuamini kuwa vyote alivyokuwa amepewa vilikuwa vyake kwa haki takatifu na kwamba yeye binafsi alikuwa Mungu wake mwenyewe. Uongo huu ulimfanya kujionyesha kuwa yeye mwenyewe alikuwa kama Aliye Juu – Baba. Lusifa hakutafuta kumuondoa Baba bali kujiwasilisha kama mwenzake asili. Hakutaka tena kumtazama Baba kupitia kwa δια lenzi ya Mwana wa Mungu. Aliwazia modeli tofauti kabisa ya usawa kwa ulimwengu ambapo wote wangejitambua kama vyanzo vyao wenyewe au ἐκ →. Hivyo Lusifa aliwazia umiliki wa ulimwengu kama:



ἐκ→ na ἐκ→
(chanzo) na (chanzo)

Fomyula hii ambaye alipendekeza ilisababisha mtiririko asili wa uhusiano wa ἐκ → δια = ζωη chanzo-njia-uzima kukoma. Nguvu za ἐκ → vyanzo viwili huru zilipelekea mvutano asili ambao unahitaji kueleweka au kusawazishwa ili kurejesha umoja tena.

Kama fomyula tunaweza ainisha hili kama:

ἐκ→ ζωη(uzima)← ἐκ
(chanzo) ↓ (chanzo)
ἐκ (chanzo)



Mgongana wa nguvu mbili za ἐκ → hupelekea kwa jumuiya au awali ya vyote viwili kwa fumbo moja. Utambulisho wa binafsi husulubishwa kwa mwafikiano wa hukumu ya mtu binafsi kwa uzuri wa kawaida, na uiano au usawa unaonekana kurejeshwa. Fomyula hii mpya inabainishwa kwa kuondoa kanuni ya δια–njia. Hivyo, ili kudumisha uiano katika ulimwengu lazima daima kuwe na mgogoro na azimio kila mtu anapopata utambulisho wa kibinafsi kwa msingi wa kuwa ἐκ→ chanzo. Lusifa ameahidi wote watakao msikiza:

> ...Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi **mtakuwa kama Mungu**, mkijua mema na mabaya. Mwanzo 3:5

Hivyo tangu mwanzo ulikuwa mango wa Lusifa kuondoa δια kuu – Mwana wa Mungu.[14] Kuwa na Mwana katika njia kungekaribisha kila mmoja kuwa sehemu ya chanzo cha jumla kupitia kwa mtindo wowote wa philosophia yoyote mtu hutamani. Kama kwa pantheism[15] au kwa Ibada ya mungu wa ulinganifu na kuwa kama yeye, haijalishi bora tu hakuna kanuni ya δια njia iliopo kwa hakika katika ukweli. Mtu anaweza jifanya kuonyesha kanunui ya δια njia bora tu ni wazi kuwa ukweli wa msingi ni ule wa ἐκ→ chanzo.

Hii ndio asili ya vita vikuu vya ulimwengu. Ni vita kati ya ufahamu huu muwili wa uhusiano wa msingi wa viumbe wa mbingu wawili wa kwanza.

| Mpangilio Takatifu wa Maandiko | Mpangilio wa Mungu wa Ulimwengu huu |
|---|---|
| ἐκ → δια = ζωη<br>Chanzo → Njia = uzima | 1. ἐκ → ζωη← ἐκ<br>(chanzo) ↓ (chanzo)<br>2. ἐκ (chanzo) |

[14] Yohana 8:44 … Alikuwa mwuaji tangu mwanzo…
[15] Pantheism ni imani ya dini yoyote au mafundisho ya filosofia ambao humtambulisha Mungu na ulimwengu au kuwa Mungu ni ulimwengu.

Mpangilio wa mungu wa ulimwengu huu ulirithiwa na waanzilishi wa taifa letu walipokubali uongo kuwa, "Hakika hamtakufa…mtakuwa kama Mungu." Mwanz 3:4,5. Hapa ndipo tulifanya biashara na nafasi yenye uiano wa δια kwa mfumo wa mgogoro wa mara kwa mara kati yetu na Mungu kuwa ἐκ → chanzo chetu wenyewe. Jinsi utaifa wetu ulifanya biashara ya δια kuu alipokuja katika ulimwengu huu na ithibati kuwa uongo huu upo kiasilia ndani ya binadamu. Alisulubishwa msalabani na kuuawa. Tabia ya upole na tamu ya Mwana wa Mungu, aliyekuwa mtiifu kwa Baba yake kwa vitu vyote haikuwa katika uiano na mawazo yaliyoanguka tuliokuwa tumerithi. Wazazi wetu wa kwanza walipokea mpangilio huu wa makufuru moja kwa moja kutoka kwa mwanzilishi Lusifa.

Inashangaza kugundua kwamba dhana ya "dialectic" ilikuwepo katika Philosophia ya Heraclitus wa Efeso (535 – 475 BCE), aliyependekeza kuwa kila kitu kinabadilika daima kama tokeo la ugomvi wa ndani na upinzani.[16] Maandiko yanafunua chanzo cha ugomzi huu wa ndani kwa kuonyesha dhana ya uongo ya Shetani kuhusu Mungu ambayo inaharibu utambulisho wa δια. Hii ndio sababu Paulo aliwaandikia:

> Hata nayo Injili yetu kama imetiwa utaji, ni kwa wale tu wanaopotea. (4) Kwa habari yao, mungu wa dunia hii amepofusha akili za wasioamini, ili wasione nuru ya Injili ya utukufu wa Kristo, aliye sura ya Mungu. 2 Wakorintho 4:3,4

Kama haiwezekani kuelewa Mpangilio Takatifu na kupata uiano wa kweli wakati ambao mawazo yetu yamepofushwa na miungu ya ulimwengu huu. Mawazo yetu yanahitaji kufanywa upya au kuzaliwa tena kwa ufahamu sahihi wa Mpangilio Takatifu.

kwa njia nyingine, tubu kwa Ibada yetu ya sanamu ya dhana ya uongo. Mfumo huu unafananishwa na kifo katika Bibilia kwa sababu ni kujisalimisha kamili na kukataa kila kitu kinachoonekana chenye mantiki na maana kinapotazamwa kupitia kwa lenzi ya Mungu wa ulimwengu huu. Njia pekee ya kurejea kwa kanuni ya δια ni kumuomba, Mwana wa Mungu, kukufunza na

[16] https://en.wikipedia.org/wiki/Dialectic#Principles

kukusaidia. Kwetu sisi wenyewe hili haliwezekani kwa sababu mawazo yetu yamepangwa kwa upande mwingine chini ya mafunzo ya Lusifa.

Kama utangulizi wa matatizo mengi "mungu wa mpangilio wa ulimwengu huu" husababisha, wacha tuangazie mtazamo haswa wa ukweli wenyewe. Ndani ya Mpangilio Takatifu "vitu vyote" hutoka kwa ἐκ → chanzo moja ambacho humaanisha kuwa kuna ukweli mmoja huru au chanzo cha ukweli. Katika kitengo hiki "mungu wa mpangilio wa ulimwengu huu" au mpangilio wa kiumbe kuna angalau vyanzo viwili vya ukweli kama tukiiga mtindo wa kuinua kila mtu kwa uungu au ἐκ → chanzo. Kwa hivyo tuko na toleo nyingi za "ukweli" na hili kimantiki hupelekea kwa upeo wa mwana falsafa wa Denmark Soren Kierkegaard (1813 – 1855) kuwa "ubinafsi ni ukweli na ukweli ni ubinafsi." Ukweli tofauti uko katika ushindani na kila moja au kuunganishwa kizushi kwa nguvu – njia yoyote mpangilio huu wa vyanzo vingi uko imara sana, na huwaangukia watu kutumia vitu vyovyote walivyo navyo katika umiliki wao kushawishi wengine kuhusu "ukweli" wao.


Vyombo viliopo vinahusisha ushawishi, udanganyifu, na hatimaye nguvu asilia za kuanzisha "ukweli" wa mtu binafsi, kwa kuwa hakuna ukweli huru katika "mungu wa mpangilio wa ulimwengu huu." Historia inadhihirisha kuwa wachezaji mashuhuri wa mtindo huu wamekuwa wale ambao wako na uwezo wa kuonyesha "ukweli" kadhaa kwa makundi tofauti, hata wakati ambao dhana hizo zinazua mgogoro. Kuonyesha "ukweli" kadhaa wa kutatanisha wakati mmoja huweka utambulisho wa msingi wa mtu kukosa thamani, kusababisha utambuzi wa mvurugano ambao hunasa mtu binafsi katika kizimba cha kukosa uwezo. Ongezeko la utata katika mfumo huu hivyo huhitaji kuzuka kwa madakatri wa kusokota kupapasa "ukweli" huu ili kupatanisha raia; na kutupa akili kwamba viongozi wengi hutetea tu kile ambacho kitazidisha sababu ya utawala wao. Wale ambao wanaweza kuwashawishi wengi kwa "ukweli" wao hata hivyo, wanaweza pata kura zinazohitajika kwa "ukweli" kutawala kundi. Mfumo wa siasa wa mataifa yote ya ulimwengu hivyo umejazwa kwa ukweli huu wa kusokota na kupapasa, na kuwaacha wahusika wakila taifa wakihisi kudanganywa na kukatishwa tamaa. Hisia hii mwishowe inaweza pelekea kwa mapinduzi na kugeuza hadhi ya utawala. Uongozi unapobadilika, matatizo hatimaye hutokea tena kwa sababu umejengeka kwa dhana sawa ya ukweli.

Wacha sasa tugeukie mgogoro huu wa ndani kuhusu kile ambacho Heraclitus wa Efeso alinena. Tutaona jinsi mafundisho ya Lusifa husababisha mgogoro katika uhusiano wa akili na mwili na vilevile katika uhusiano wa fikira na hisia.

# 8. Sabato kwa nafsi: Kupata Pumziko la Ndani

Kisa cha Bibilia cha uumbaji wa mwanadamu kinadhihirisha kuwa:

> ...Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai. Mwanzo 2:7



Hivyo tunajifunza kuwa mtu ni muunganiko wa mwili na pumzi/hewa/roho. Hivyo basi kuna uhusiano upi kati ya hivi viwili vya mwili na roho au mwili na akili? Ukitafuta kwenye mtandao istilahi "Mind Body Problem" utajua kuna mwili mzima wa fasihi ambao umejitolea kujibu swali hili.

> Moja ya maswali makuu katika saikolojia (na filisofia) kuhusiana na tatizo la akili/mwili: ni akili ni sehemu ya mwili, au mwili sehemu ya akili? Kama ziko tofauti, basi zinahusiana aje? Na ni gani kati yazo mbili inamiliki?[17]

Wacha tujaribu maswali haya katika mipangilio miwili ambayo tumekuwa tukielezea.

| Mpangilio Takatifu wa Maandiko | Mpangilio wa Mungu wa Ulimwengu Huu |
|---|---|
| ἐκ → δια = ζωη<br>Chanzo → Njia = Uzima | 1. ἐκ → ζωη← ἐκ<br>(chanzo) ↓ (chanzo)<br>2. ἐκ (chanzo) |

Kutambua mambo katika Mpangilio Takatifu ni rahisi tu wakati ambao tunatumia tabia zisizoonekana na zinazoonekana. Ni wazi akili hazionekani na mwili unaonekana. Hivyo basi fomyula katika muktadha huu ni:

Akili → mwili = uzima

Kama tukitumia tabia husika za mpangilio tunaona kwamba akili ni kichwa au kiongozi cha mwili. Mwili ni njia ambayo akili inadhihirishwa. Mawazo ya akili

[17] http://www.simplypsychology.org/mindbodydebate.html

yanawekwa wazi kupitia kwa sauti na matendo ya mwili. Mtume Paulo alionyesha uhusiano huu wa akili–mwili aliposema

> ...nautesa mwili wangu na kuutumikisha ili nikishawahubiria wengine, mimi nisiwe mtu wa kukataliwa. 1 Wakorintho 9:27

Mwili umewekwa chini ya akili. Lakini katika hatua hii lazima tuwe makini ili kwamba tuambatane na sifa za Mpangilio Takatifu. Akili ni mlinzi wa mwili kwamba akili hutaka kula vizuri, kufanya zoezi, na kupumzika vyakutosha kwa mwili. Hili ni kinyume cha maoni ya Plato yaliyopelekea kwa kukandamizwa kwa mwili na kuchipuka kwa monaki[18] na kupigwa kwa mwili. Wazo hili ni moja ya mpangilio wa kiumbe kama tutakavyotambua. Katika mfano huu tunaona:

1. Akili→ uzima ← Mwili (Uwili)
   Au
2. Akili/Mwili (Umoja)[19]

Wakati akili na mwili vinaeleweka kama vyombo viwili vya chanzo, kutakuwa na tokeo la juhudi ya kuleta uiano kwa vitu hivi viwili kinzani. Moja ya hali ya kawaida ya mwanadamu ambayo hutokea kwa mpangilio huu wa uzima ni jinsi ya kukabiliana na swali la njaa. Wakati mwili unatoa ishara ya njaa na uko hadhi sawa na akili, basi ni gani huamua nini na ni kiasi gani kitaliwa? Kwa njia nyingine, kujieleza kwa njaa kwa mwili ni wito au amri? Katika Mpangilio Takatifu inaeleweka kama wito kwa akili. Akili hutathmini kama ombi litafanikiwa au kudhuru mwili na kisha hutoa agizo. Kama utenda kazi wa mwili utatii akili inaposema la, hakutakuwa na mgogoro, lakini kama mwili, haswa sehemu ya chini ya ubongo, haiko chini ya sehemu ya mbele ya ubongo, kutakuwa na vita katika akili kula au kutokula. Vita hivi vinapiganwa katika kiwango kikubwa cha ulimwengu wote kupitia kwa masuala na fetma na magonjwa mengi ya mtindo wa maisha ambayo hutendeka kwa sababu akili imedunishwa nafasi ya kiwango cha pili kwa mwili.

Katika Mpangilio Takatifu, uiano wa akili na mwili unapatikana katika utawala wa akili juu ya mwili ambapo akili hutunza mwili na kuulinda, na mwili hulea

---

[18] Monaki ni mtindo wa maisha ambao kwao mtu hukataa ushawishi wa ulimwengu ili kujitoa kwa kazi ya kiroho. Utendaji Monaki mara nyingi huhusisha taaluma ngumu kupitia kwa mateso ya mwili ili kudhoofisha na kukandamiza tamaa ya mwili.
[19] https://en.wikipedia.org/wiki/Mind-body_problem

akili na kukuza mawazo yake na matakwa. Mradi tu akili na mwili umepangiliwa kwa mpangilio mkuu wa fomyula ya ἐκ → δια chanzo-njia, itataka kutenda katika mpango huu na hivyo kuzuia vita ndani ya nafsi, na kuleta pumziko. Ni sifa za Mwana wa Mungu, δια kuu ya ulimwengu, ambao huhakikisha pumziko. Kama Yesu alivyofundisha:

> Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Mathayo 11:28


Uiano wa akili na mwili unaweza anza kuja tunaporuhusu kanuni ya δια Kristo kuingia maishani mwetu kuathiri masuala ya njia ya uumbaji wetu. Uiano huu hupelekea kwa tokeo katika Sabato au pumziko kwa nafsi.

Suala la akili na mwili linaweza panuliwa zaidi katika uhusiano wa fikira na hisia. Wacha tutumia fomyula zote mbili tena. Kidokezo chetu cha Mpangilio Takatifu ni kuwa sababu haionekani na mhemko huhusisha dhihirisho linaloonekana.

**Fikira→ Hisia = Uzima**

Kinyume chake ni "kuwa-mungu-wako-mwenyewe" mpangilio wa kiumbe huu huwa:

1. Fikira→ Uzima ← Hisia
↓
2. Utawala wa Fikira "umantiki."[20]
AU
2. Utawala wa Hisia "Wacha hisia zikuongoze."




Kama ukifanya kiwango chochote cha utafiti juu ya fikira na hisia, utapata mawaidha mengi ya jinsi ya kuleta uiano kwavyo. Kwa kutambua fikira na hisia kama vyanzo viwili vikitazamwa kama kanuni pinzani, kunaumbwa vita vya ndani vya utawala. Plato alionyesha hili kama farasi maisha meupe na meusi wakivuta mkokoteni wetu wa maisha. Kwa Plato, farasi mweupe alikuwa fikira na mweusi alikuwa hisia, hivyo kupendekeza hali pinzani ya uhusiano.

[20] https://en.wikipedia.org/wiki/Chariot_Allegory

Upinzani mweupe na mweusi ulienda hatua zaidi katika Mashariki kwa kanuni ya Yin na Yang ambayo kwayo moyo wa mweupe ni mweusi na moyo wa mweusi ni mweupe. Tena tunaweza pata sehemu ya onyesho la hili katika mfululizo wa sinema ya *"Star Wars"* ambapo moyo wa maadili wa Jedi ulionyeshwa kwa utulivu, nidhamu iliyopangwa ikiongozwa na hisia za mmoja.

Mtu anaweza jibu kuwa katika moyo wa hisia kuna fikira, lakini hili hufunga mzunguko wote wa lugha unaomuongoza mtu kwa kujirudia kwa ajabu, uwepo usio fahamika. "Waliopata mwanga" wakati mmoja wanakwambia kuwa kuuliza ni kudhihirisha hali yako ya mawazo ya kutofahamu; lazima tu uache moyo wako ukumbatie kile ambacho akili zako haziwezi kubali. "ni siri; ikubali tu ."




Utata huu wote, mgogoro, na vita vinaweza pumzishwa kwa kukubali Mpangilio Takatifu na wa uongozi wa utiifu wa uongozi wa fikiria na hisia ambapo hisia hutenda kama utukufu na mng'ao wa utukufu wa akili. Mwana wa pekee anatwalika kula mkate mkuu wa δια ya uzima kurejesha uiano wa Kweli na kuleta pumziko kwa akili na miili yetu.

## 9. Njia Nyembamba ya kwenda kwa Mpangilio Takatifu



Umewahi tazama mtu akiruka katika mchezo wa “base jump” kutoka jabali refu au jumba? Kuruka (Base Jumping) ni mchezo uliokithiri ambao unaruka kutoka mahali makini zaidi na hatari na kisha kutumia parashuti kabla ya kuanguka ardhini. Nimetazama video kadhaa kwenye mtandao ambazo zimerekodi uzoefu huu. Warukaji husimama juu ya kikwazo cha hofu ambayo lazima uishinde ndiposa uruke. Kufanya mpito kutoka kwa “mpangilio wa mungu wa ulimwengu” hadi kwa Mpangilio Takatifu ni sawa na mchakato huu. Kama tukionyesha fomyula ya Mpangilio Takatifu katika Muktadha wa mlima takatifu wa Mungu, ambapo Baba anakaa juu ya Mlima tunaona yafuatayo:




Chanzo

Njia


Bibilia inatwambia kuhusiana na Baba:

> Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu, Isaya 57:15

Baba anakaa mahali palipoinuka, na kumfikia kwote na kupitia δια kwa Mwanawe. Mwana wa Mungu anashikilia nafasi ya unyenyekevu na utiifu kwa Baba yake. Mwana alirithi kila kitu ambacho Baba alikuwa nacho, lakini anasalia mtiifu na chini ya utawala wa Baba. Lusifa, ambaye alifanyika Shetani baada ya anguko, alitamani kupanda mpaka mbinguni na afanane na yeye Aliye Juu.

> Nawe ulisema moyoni mwako, Nitapanda mpaka mbinguni, Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, Katika pande za mwisho za kaskazini. (14) Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu.' Isaya 14:13-14

Mwendo huu wa kujiinua nafsi unaweza onekana ifuatavyo:




Chanzo ↔ chanzo

Kutafuta kujiinua ili kuwa sawa na Mungu, na kuketi katika hekalu la Mungu na kudai kuwa Mungu ni kutafuta cheo cha juu zaidi. Cheo hiki sio chetu na kwa hivyo hutuweka katika mpaka wa jabari refu sana. Kurejea katika cheo chetu cha kweli katika utiifu kwa ἐκ → Chanzo kuu cha ulimwengu kunahitaji turuke kutoka kwa cheo hiki. Kama tukifanya kuruka huku sisi wenyewe tutakufa na kupotea milele. Kuna kiumbe mmoja ulimwenguni ambaye angeruka na kutufungulia njia ya kurejea mahali barabara pa Mpangilio Takatifu. Mwana wa Mungu alifanywa kuwa sawa na Baba yake. Amepewa haki ya kusimama juu ya mlima pamoja na Baba yake. Lakini kwa kuhurumia taifa letu lililoanguka, Kristo alifanya mruko wa kushangaza, ili kwamba aweze kuturejesha katika uhusiano wa kweli na Baba.

> Tuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Kristo Yesu. (6) Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho, (7) bali alijifanya si kitu, akajifanya sawa na mtumwa, akazaliwa katika umbo la mwanadamu. (8) Naye akiwa na umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba! Wafilipi 2:5-8

Katika kuruka kukubwa kutoka mlimani, Mwana wa Mungu alitufungulia njia ya kurejea kwa Mpangilio Takatifu na kujifunza tena kanuni za δια Mwana wa Mungu. Changamoto kwetu ni kwamba hatuna parashuti, na kuruka kwetu bila shaka ni kwa kifo chetu. Kutoka juu haiwezi onekana kwamba tunaporuka Kristo anaweza kutushikilia hadi tufike chini, na huchukua athari za kuanguka kwa niaba yetu kwamba kwa kufa mara moja, alikufa mara moja kwa wote.

Bali hamu ya kuruka huja tu kwa wale ambao hutambua kuwa ni makufuru kutafuta pahali patakatifu pa Mungu mwenyewe. Katika hali yetu halisi hatuoni tatizo lolote na hali hii kwa kuwa Mungu wa ulimwengu huu amepofusha macho yetu kwa makufuru haya ya kutisha. Amri ya Mungu inasikika kutoka mlimani,

> Usiwe na miungu mingine ila mimi. Kutoka 20:3

Tunapoona umeme, kusikia radi, na kuhisi milima ikitetemeka, tunafanywa kuhisi hatari ya nafasi yetu. Tunahisi haja ya kuruka, lakini tunaogopa kwamba tunaweza kufa, na kwa hivyo tunasalia kuganda katika mahali hatari juu ya mlima. Ukweli ni kwamba sababu tu ambayo tunaweza kuwa hai ni kwa ajili ya ombi la Mwana akiwa msalabani, "Baba, wasamehe; hawajui walitendalo."

Kukanyaga mlimani kunafaa kumaanisha kifo cha papo, kwa sababu tunapotafuta kujiinua tunapaswa kuanguka mara hiyo kwa kifo chetu. Hata hivyo, Kristo anatuombea kwa Baba atupe muda wa kuweza kutambua dhambi hii yetu kuu. Tutakapo ona tu ndio itawekwa juu yetu, kupitia kwa Sheria ya Mungu, kukimbilia mikononi mwake na kuruhusu nafsi zetu zisulubiwe pamoja naye na kuzaliwa upya katika δια uzima. Tunajipata kama wazazi wetu wa kwanza, tukiwekwa kwa utiifu chini ya mlima na kusubiri kwenda juu tuitwapo, tukivikwa katika mavazi ya δια njia ya Mwana wa Mungu.

Mahali pa kuruka kutoka mlimani katika maandiko panaitwa mlango mwembamba. Hapa ni mahali pembamba sana ambapo tunaweza hisi kumbatio la Mkombozi na turuke naye.

> Ingieni kwa kupitia mlango mwembamba, kwa maana lango ni pana na njia ni pana ielekeayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa kupitia lango hilo. Mathayo 7:13

Mlango mwembamba ni mgumu kuupata na vilevile kuingia kwa watu wengi. Kwanza ni vigumu kuupata kwa sababu hatuhisi kwa uasilia hitaji la kuingia. Mara tu tunapopata lango, mlango mwembamba huhitaji tuache kila kitu katika maisha haya ili kuupitia. Lazima tuwe tayari kuwa kama ngamia ambaye atapitia tundu la sindano. Sindano ilikuwa fupi, tundu nyembamba katika ukuta wa mji wa Yerusalemu. Malango makuu yalipofungwa hii ndio ilikuwa tu sehemu ambayo Mtu angepitia. Tajiri angehitajika kushusha hazina yote kutoka kwa ngamia na kumfanya apige magoti na kuchanga kupitia kwa tundu kwenye ukuta. Hii ndio maana ni vigumu kwa tajiri (yule ambaye anakiburi ndani yake mwenyewe na anajiinua na kushikilia "mambo" yote yanayomwasilisha kama mwenye thamani) kuingia kwa mlango mwembamba. (Matt 19:24)

Sheria inaposikika kutoka mlimani kwa onyo la upendo, uongo wa kulevya ambao ni wetu wenyewe ἐκ → chanzo husababisha wengi kufanyia mzaha maonyo kama hayo kama uongo ambao umeundwa kuhofisha na kutawa

wasio salama. Wengine hufunza kuwa sheria sio muhimu tena, kwa sababu yote yalitimizwa na kukamilishwa msalabani. Kuruka kwa kufedhehesha kwa Kristo kwa kifo chake kulitosha; hatuhitaji kuruka naye. Hatuhitaji kujinyenyekesha na kutubu katika namna ya moyo unaoumiza kama huo. Kupitia kwa uvumbuzi huu na vumbuzi nyingine nyingi mlango mwemba umefunikwa na kufichwa kwa ulimwengu, ili kwamba mtu asalie akivuliwa katika δια mavazi ya Mwana wa Mungu.

Wale ambao wanapatwa bila mavazi katika mlima wakati wa harusi ya Mwana wa Mungu kwa Kanisa watahitajika kuruka kutoka mlimani peke yao. Mara na nyingine Mwana wa Mungu alimwita kondoo aliyepotea mlimani, akienda mbali kuwakusanya kondoo waliopotea tena, lakini hawakumsikia. Kilio kilisikika, "Hatutaki mtu huyu atawale juu yetu." Hivyo basi wataruka peke yao bila mpatanishi, na itadhibitisha kutokuwa na umuhimu kabisa.



Kusimama juu ya jabali na kutazama chini maelfu ya fiti huonekana ngumu sana. Huhisika kuwa hakika lazima tutakufa, lakini Yesu ametwambia:

Mtu ye yote anayependa maisha yake atayapoteza, naye ayachukiaye maisha yake katika ulimwengu huu atayaokoa hata uzima wa milele. Yohana 12:25

Je, unataka furaha na mafanikio ambayo yatukuwa yako kama utaingia katika Mpangilio Takatifu na kugundua ufunguo ambao hurejesha, huleta uiano, na hufungamanisha mahusiano yote ambayo yanakuhusu? Wacha sheria ya Mungu inene katika nafsi yako, wacha macho yako yafunguke kwa uovu wa kuamini kuwa we ni ἐκ → chanzo chako mwenyewe. Kama hauwezi ona jinsi huu ni uzoefu wa kawaida uliorithiwa kutoka kwa wazazi wetu wa kwanza, omba upewe macho ya kuona na kugundua uchungu wa mahusiano yaliyovunjika na vita vya ndani ambavyo virusi vya mpangilio wa viumbe unavyo rarua mawazo na mwili wako. Kuja kwa mlango mwembamba na uachilie vitu ambavyo umeshikilia kwa vile vinakuelezea sasa, na kuona kwa Kristo yule ambaye hawezi kukuacha wala kukukana juu ya asili

yako katika bonde la unyenyekevu. Yesu anaelezea njia ya baraka. Nakukaribisha ujifunze kwa makini na ukumbatie kila hoja.

Kisha akafungua kinywa chake akawafundisha, akisema:

> (3) “Wana heri walio masikini wa roho, maana hao Ufalme wa Mbinguni ni wao. (4)Wana heri wale wanaohuzunika, maana hao watafarijiwa. (5) Wana heri walio wapole, maana hao watairithi nchi. (6) Wana heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watatoshelezwa. ( 7) Wana heri wenye huruma, maana hao watapata rehema. (8) Wana heri walio na moyo safi, maana hao watamwona Mungu. (9) Wana heri walio wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu. (10) Wana heri wanaoteswa kwa sababu ya haki, maana hao Ufalme wa Mbinguni ni wao. (11) Mna heri ninyi watu watakapowashutumu na kuwatesa na kunena dhidi yenu mabaya ya aina zote kwa uongo kwa ajili yangu. (12) Furahini na kushangilia kwa maana thawabu yenu ni kuu. Mathayo 5:3-12

Yesu anasema:

> Njooni kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Mathayo 11:28

Inaweza chukua siku kadhaa za kutafuta moyo wako. Unaweza kuwa hata ukijifikiria kuwa unatembea katika njia ya Kristo lakini sasa kuwa katika vita na nafsi kumezalisha matokeo machache katika tabia yako. Leo ndio siku ya wokovu. Kristo yuko tayari kukushika mkono na kukubeba katika bonde. Nakukaribisha uchukue hatua hii na uvune mazao ya imani, sio mazao ya ujinga, ila mazao katika itikio la maarifa kamilifu ya njia mbaya ambayo sote tumekuwa tukiishi kwayo. Najua hautajutia uwaamuzi huu. Yesu anatwambia hivi leo:

> Wale wote anipao Baba watakuja Kwangu na ye yote ajaye Kwangu, sitamfukuzia nje kamwe. Yohana 6:37

## 10.Hatua Ifuatayo

Katika kijitabu hiki kidogo baadhi ya kanuni za msingi za Mpangilio Takatifu zimewasilishwa. Sasa kuna uvumbuzi wa ulimwengu ambao unakusubilia wa vile mfungamano wa chanzo na njia katika sehemu zote za Maisha yako zinaweza patikana kwa Baba na Mwana. Huu ndio mwanzo wa mfululizo wa vijitabu vinavyoonyesha masuala ya Mpangilio huu Takatifu. Katika safari yetu tunataka tutembelee Mpangilio Takatifu wa upendo, Mpangilio Takatifu wa ndoa, Mpangilio Takatifu wa sheria, Mpangilio Takatifu wa ibada, Mpangilio Takatifu wa fedha. Nakushukuru kwa kuwekeza kwa safari hadi u mbali huu, na ninaomba kuwa imekuwa mbaraka kwako. Maneno haya ya Baba yetu yanaweza kuzungumzia:

> Mwanangu, kama ukiyakubali maneno yangu, Na kuyaweka akiba maagizo yangu; (2) Hata ukatega sikio lako kusikia hekima, Ukauelekeza moyo wako upate kufahamu; (3) Naam, ukiita busara, Na kupaza sauti yako upate ufahamu; (4) Ukiutafuta kama fedha, Na kuutafutia kama hazina iliyositirika; (5) Ndipo utakapofahamu kumcha Bwana, Na kupata kumjua Mungu. (6) Kwa kuwa Bwana huwapa watu hekima; Kinywani mwake hutoka maarifa na ufahamu; (7) Huwawekea wanyofu akiba ya hekima kamili; Yeye ni ngao kwao waendao kwa ukamilifu; (8) Apate kuyalinda mapito ya hukumu, Na kuhifadhi njia ya watakatifu wake. Methali 2:1-8

> Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye kwa Yeye (δια) vitu vyote vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi. 1 Wakorintho 8:6

> MeYesu akawaambia, "Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia (δια) Kwangu." Yohana 14:6

> Kwa hiyo Yesu akasema nao tena akawaambia, "Amin, amin, nawaambia, Mimi ndimi lango la kondoo. (8) Wote walionitangulia ni wevi na wanyang'anyi, lakini kondoo hawakuwasikia. (9) Mimi ndimi lango, ye yote anayeingia zizini kwa kupitia (δια) Kwangu ataokoka, ataingia na kutoka, naye atapata malisho. Yohana 10:7-9

> ...sisi tunamhubiri Kristo aliyesulibiwa, ambaye kwa Wayahudi ni kitu cha kukwaza na kwa Wayunani ni upuzi. (24) Lakini kwa wale ambao Mungu amewaita, yaani, Wayahudi na Wayunani, Kristo (δια) ni nguvu na hekima ya Mungu. 1 Wakorintho 1:23-24

> ...ili wapate kujua ulivyo utajiri wa ufahamu kamili, waijue siri ya Mungu, yaani, Kristo mwenyewe, (3) ambaye ndani Yake kumefichwa hazina yote ya hekima na maarifa. Wakolosai 2:2-3

# Mpangilio Takatifu Wa Maisha

**Mipangilio ya mambo yote** ya maisha inatuzunguka.
Inatoka kwa Mpangilio Takatifu asilia unaoshuka kutoka kwa Baba, kupitia kwa Mwana, unaopatikana katika kila ngazi ya maisha.

Jua na mwezi, mbegu na mimea, wazazi na watoto, mfalme na nchi,
Agano la Kale – Agano Jipya, mpangilio wa Chanzo na Njia ndio muhimu.

Kwa kinyume, cha kuhujumu, mpangilio wenye mgogoro umejipenyeza katika maisha ya waume, na wake, na mioyo na mawazo ya watawala na viongozi. Wote lazima wachague mpangilio wao wa uzima au mauti. Maandiko matakatifu yanatuhimiza tuchague uzima.